Kufanya Mageuzi ya Afya ya Akili ya Utotoni na Watoto Wachanga

UCHAMBUZI WA MAZINGIRA NA MPANGO MKAKATI WA KING COUNTY

King County
Best Starts for KIDS

SEHEMU YA 1: **Muhtasari kwa Jumuiya**

Dondoo za “Kufanya Mageuzi ya Afya ya Akili ya Utotoni na Watoto Wachanga”

Mahusiano ni kiini cha maendeleo na ustawi wa binadamu

Kwa watoto wachanga, watoto wanaoanza kutembea, na watoto wadogo, maendeleo yote yanatokea katika mahusiano. Mahusiano kati ya watoto na walezi wao yanatoa msingi wa kijamii na kihisia unaohitajika kwa watoto ili kujifunza na kustawi katika maisha yao yote.[1] Sekta changa ya **Afya ya Akili ya Utotoni na Watoto Wachanga** inatoa maelezo mengi muhimu ili kuhakikisha watoto wanastawi katika kila familia ya King County.

Muhtasari huu kwa jumuiya ni maelezo mafupi ya ripoti yetu ndefu iitwayo Kufanya Mageuzi ya Afya ya Akili ya Utotoni na Watoto Wachanga: Uchambuzi wa Mazingira na Mpango Mkakati wa King County.

Mwaka 2017, Best Starts for Kids ilifanya ***uchambuzi wa mazingira*** ili kutambua uwezo, fursa na changamoto za huduma za Afya ya Akili ya Utotoni na Watoto Wachanga katika King County. Uchambuzi huu ulizaa **mpango mkakati** ili kuunga mkono suala la kuboresha matokeo ya kijamii na kihisia kwa watoto na familia. Kwa kutekeleza mpango mkakati huu, tunakusudia kuimarisha huduma za Afya ya Akili ya Utotoni na Watoto Wachanga katika King County.

Muhtasari Wetu

Dira na maadili

Dira ya Best Starts ni kumsaidia kila mtoto anayezaliwa au anayelelewa King County kufika utu uzima akiwa na furaha, afya, salama na ustawi. Kwanza, wanajumuiya walianza kwa kuandaa dira na maadili ya pamoja ili kuongoza uchambuzi na mchakato wetu wa kuweka mipango.

Tunaiona King County inayothamini jitihada za familia za kutengeneza mazingira yenye kuwajali watoto. Kuelekea lengo hili, King County inazidisha kuipa kipaumbele afya ya kijamii na kihisia ya watoto wachanga, watoto wanaoanza kutembea, na watoto wadogo (wachanga hadi miaka 5) na familia zao.

Maadili ya msingi na dhamira za mradi huu ni pamoja na **haki, wajibu na uaminifu, huduma zinazozingatia binadamu, ushirikiano na ujumuishaji**.

Mchakato wetu

Mradi huu ulitumia mbinu iitwayo “utafiti wa shughuli za Jumuiya.” Kuanzia Januari 2019 hadi Juni 2021, tulikusanya simulizi kutoka kwa makundi mbalimbali ya familia, watoa huduma, na wabia wa jumuiya. Kwa simulizi hizi, tulifanya kazi pamoja na familia na wabia wa jumuiya ili kuleta maana, kuweka vipaumbele, kuweka mipango na kufanya mapitio ya ripoti hii. Tulifanya kazi katika mazingira mahalia sambamba na wabia wa King County na mradi kama huu unaoshirikisha jimbo lote.

Familia nyingi za King County zilishirikishwa katika mradi huu, ikiwa ni pamoja na:

Familia 7 mahsusi kwa utafiti ili kuzingatia mawazo ya familia za Weusi, Wazawa, Walatini, Wakongo na Wavietnamu.

Baraza la Jumuiya lenye Wajumbe 12 la wazazi na watoa huduma wa King County ili kushirikishana picha na simulizi za maisha yao binafsi na uzoefu wao wa Afya ya Akili ya Utotoni na Watoto Wachanga.

Afya ya Akili ya Utotoni na Watoto Wachanga ni nini?

Katika kiini cha Afya ya Akili ya Utotoni na Watoto Wachanga kuna uwezo mkubwa wa watoto wadogo. Tunataka kuimarisha uwezo wao wa:

- kutambua, kuelezea, na kudhibiti hisia zao;
- kutengeneza mahusiano ya karibu na watoto wengine na walezi; na
- kuvumbua na kujifunza katika familia zao, jumuiya yao na utamaduni wao.[2]

Familia na watoa huduma za afya, pamoja na vitongoji, makundi ya kijamii, programu za ujifunzaji wa awali, na jumuiya kwa ujumla—watu na maeneo katika maisha ya watoto vyote hivi vina mchango katika maendeleo na ustawi wao wa kijamii na kihisia.

Familia zote zinahitaji kuungwa mkono ili kuwapa watoto msingi thabiti wa kijamii na kihisia

Uzoefu wa kulea watoto unaweza kuleta furaha na manufaa, pamoja na kuleta mfadhaiko na changamoto. Mahusiano ya kifamilia yanaanza kabla ya mtoto kuzaliwa na yanaendelea kwa maisha yake yote.

"Mwendelezo wa malezi" unahusisha mambo mengi

Uendelezaji

Kuendeleza utambuzi huhusisha usaidizi kama vile kushirikishana taarifa, kupima ukuaji, na rasilimali zinazosaidia uhusiano thabiti kati ya mtoto na mlezi, ukuaji mzuri, na ujifunzaji wa awali. Watoto na familia zote zinahitaji ufikio wa suala la uendelezaji wa Afya ya Akili ya Utotoni na Watoto Wachanga.

Uzuiaji

Unahusisha huduma zinazosaidia kushughulikia na kupunguza wasiwasi wa maendeleo ya kijamii na kihisia na zile zinazoendeleza uwezo wa watoto wadogo na familia zao.

Utabibu

Unahusisha huduma za kitabibu zinazoshughulikia vyanzo vya majeraha ya akili na mvurugo wa ustawi wa kijamii na kihisia. Kupunguza huzuni na kuongeza uthabiti na kupona huwasaidia watoto wadogo na familia zao kurejea katika ukuaji mzuri.

Uchambuzi Wetu wa Mazingira

Kuwepo ... SIMULIZI YA SELAM

"Wakati tulipokuwa tukitembea bega kwa bega kuelekea eneo lake la kufanyia mazoezi, Josiah aliniangalia na kusema, 'Nakupenda mama.' Niliguswa sana moyo kwa sababu kulikuwa na mambo mengi niliyokuwa nikiyahofia na ndipo ikanilazimu kuweka mkazo katika jambo la muhimu: kuwepo na kutumia muda vizuri na mwanangu.

Kama mama anayelea mtoto peke yake na mfanyakazi, kuna mambo mengi naogopa kukosea: kutotumia muda naye, kutompa anachohitaji, au kwamba kuna kitu anakikosa. Najua siko peke yangu. Kazini nasikia mambo kama haya kwa akina mama naofanya nao kazi. Kuna hofu kwa kila mmoja ya majeraha ya akili waliyoyapata na jinsi gani jambo hili linaweza kuwa na madhara ya muda mrefu. Nyakati kama hizi ni muhimu sana kuzizingatia."

—mzazi wa King County

Watoto wadogo na familia za King County ni kina nani?

- **Takribani watoto 130,000** chini ya miaka 5 wanaishi King County.[3]
- **Katika miaka 10 iliyopita,** anuai ya mbari za watoto wadogo wa King County imeongezeka.
- **Zaidi ya asilimia 20 ya wakazi** wa King County ni wahamiaji au familia za wahamaji.[4]
- **Zaidi ya watoto 18,000** chini ya miaka 5 (asilimia 14.6) wa King County wanaishi katika umaskini.[5]
- **Mjamzito 1 au zaidi kati ya 4** wa King County anapitia mfadhaiko wa kuzaa.[3]
  Utafiti unaonesha kwamba magonjwa ya akili, wakati na baada ya ujauzito, ni jambo la kawaida kwa watu wanaojifungua na linaweza kusababishwa na mabadiliko ya kimwili na homoni pamoja na athari za kihisia za kiumbe hiki muhimu.[6]



> *"Tunajitahidi kuendeleza urithi wetu kwa kuwashirikisha watoto wetu utamaduni wetu mzuri hata pale jamii inapojaribu kutuambia vinginevyo"*
>
> *- mzazi wa King County*

Familia za King County zina uwezo mkubwa wa kuwasaidia watoto wao wadongo, ikiwemo:

- Elimu ya malezi ya watoto.
- Kusoma, kuimba, na kuwapa watoto wao fursa za kujifunza.[7]
- Kuwa na mtu wa kumwomba ushauri wa usaidizi wa kihisia kuhusiana na uzazi au kulea watoto.[8]

Lakini bado kuna changamoto za ufikio wa huduma za Afya ya Akili ya Utotoni na Watoto Wachanga, kama vile:

- Familia na watoa huduma si wakati wote wanajua pa kupata taarifa au huduma.
- Si huduma zote zina ubora, zinazingatia tamaduni, au zinapatikana kwa lugha inayopendelewa na familia husika.
- Hakuna huduma za kutosha kukidhi mahitaji ya familia katika kaunti yote.
- Usafiri, saa zisizo rafiki, kusubiri kwa muda mrefu, na michakato ni mambo yanayoleta vikwazo.
- Huduma zinahitaji kuratibiwa vizuri ili kukidhi mahitaji ya watoto na familia zao.

Kihistoria, baadhi ya watoto na familia zinapata changamoto zaidi za kufikia huduma za Afya ya Akili ya Utotoni na Watoto Wachanga. Katika mifumo ya sasa, Weusi, Wazawa, familia za watu wa rangi mbalimbali, wahamiaji, watu wasiozungumza Kiingereza, na familia zilizo vijijini zinaweza kuwa na changamoto za kupata mahitaji yao.

Mpango Mkakati Wetu

Familia nyingi na wabia wa jumuiya walisaidia kuleta maana na kuweka vipaumbele vya gunduzi kutoka kwa makundi mahsusi ya utafiti. Vipaumbele vitano vinatokana na dira na maadili yao. Kila kupaumbele kina mikakati kadhaa na hatua muhimu zilizoainishwa katika mpango mkakati mrefu zaidi. Kupitia hatua hii ya kwanza, tunatumaini kuleta mabadiliko hitajika katika Afya ya akili ya Utotoni na Watoto Wachanga.

KIPAUMBELE CHA 1: Kuendeleza ustawi wa kijamii na kihisia kwa watoto na familia zote.

KIPAUMBELE CHA 2: Kuunganisha familia zaidi kwenye huduma za Afya ya Akili ya Utotoni na Watoto Wachanga, ikiwemo, uendelezaji, uzuiaji, na utatibu.

KIPAUMBELE CHA 3: Kutoa huduma zenye ubora wa hali ya juu, zinazozingatia tamaduni na ambazo zinakidhi mahitaji ya familia.

KIPAUMBELE CHA 4: Kuunga mkono watoa huduma wote wa mwendelezo wa malezi.

KIPAUMBELE CHA 5: Kujenga na kuimarisha mtandao wa huduma za Afya ya Akili ya Utotoni na Watoto Wachanga katika kaunti yote.

Kufanya Mageuzi ya Afya ya Akili ya Utotoni na Watoto Wachanga: Uchambuzi wa Mazingira na Mpango Mkakati wa King County

Mradi huu ni jitihada ya miaka mingi ya kusikiliza, kujifunza, na kuweka vipaumbele. Mikakati pendekezwa inawazingatia watoto na familia na italeta mabadiliko makubwa na endelevu baada ya muda fulani. Tunalo tumaini kubwa kwamba kazi yetu ya mbeleni itaendana na familia, watoa huduma, na wabia wa jumuiya. Watenda kazi wengi wa Afya ya Akili ya Utotoni na Watoto Wachanga wanahitajika ili kuitikia wito huu wa kuchukua hatua.

2106_11561a_iecmh_lasp_community_summary_SI.indd